# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA WAZIRI MKUU

## TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**Namba za Simu**

**Mkuu wa Shule: 0788605075**

**Makamu M/wa Shule: 0786226927**

**Mtaaluma 0785060949**

**Matron: 0752582235**

**Shule yaSekondari Mondo,**

S.L.P 88, Chemba,

Tarehe ..............................

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**………………………………………………

**S.LP ……………………………………………...........................................**

Yah:**MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MONDO HALMASHAURI YA WILAYA YA CHEMBA MWAKA .................................**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka .............. na atasoma tahasusi ya ………….

Shule ya Sekondari Mondo ipo Tarafa ya Mondo,Wilaya ya Chemba na Mkoa wa Dodoma.
Unaweza kufika shuleni Kwa kupanda basi stendi ya Chang'ombe au ya Machame iliyopo Dodoma mjini Kila siku saa 4:30 asubuhi na utashuka stendi ya Mondo umbali ikiwa ni km 137 sawa na nauli ya Tsh 10000/=. Aidha unaweza kufika Mondo kutoka stendi ya Mabasi Kondoa Mjini umbali ikiwa ni km 20 sawa na nauli ya Tsh 3000/= na utashuka stendi ya Mondo.Kutoka hapo utatembea Kwa mguu mwendo mfupi wa mita 400 kufika shuleni.
Muhula wa Masomo unaanza tarehe ................... hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe ..................., Mwisho wa kuripoti ni Tarehe...............

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia**

**Mwanafunzi anatakiwa kuja na sare/mahitaji yafuatayo:-**

a) Mashati mawili(2) meupe au zaidi ya mikono mirefu yenye mfuko mmoja na yasiyo bana mwili(mashati ya tomato) Kwa wanafunzi wa kiislamu waje na JUBA mbili (2) nyeupe ndefu zenye kufunika kifua mpaka kwenye vifundo vya mikono na zisizo na urembo wowote.

b) Sketi mbili (02) au zaidi za rangi ya bluu nyeusi **(dark blue) mshono wa RINDA BOX kubwa mbele na nyuma na mawili kushoto na kulia na tai mbili zenye rangi ya sketi (dark blue), urefu wa sketi ufike kwenye vifundo vya miguu kitambaa kizito Cha suti.(ni marufuku mwanafunzi kuwa na sketi fupi)**

c) Viatu vya rangi nyeusi vya **kufunga na kamba** na visiwe na visigino virefu pamoja na soksi ndefu nyeupe jozi mbili au zaidi.Haturuhusu viatu vingine vyenye urembo wa aina yeyote .

d) Nguo za michezo ambazo ni Track suit ya rangi ya blue bahari (light blue) jozi moja au Zaidi (atavaa wakati wa maandalio ya usiku na michezo).

e) Sweta moja rangi ya bluu nyeusi ( dark blue) inayofanana na sketi za shule.

f) Kwa wanafunzi wanaosumbuliwa na Athma kwaajili ya kuzuia baridi waje pullneck nyeusi

g) Nguo za kushindia gauni la draft ndogo ya dark blue refu lifike kwenye kifundo cha mguu, kwa anayehitaji kununua shuleni litapatikana katika maduka jirani na shule kwa shilingi elfu ishirini na tano tu (25000/=),(mshono solo). Fulana (T-shirt) mbili (02) za bluu zenye kola na nembo ya shule kwa anayehitaji kununua shuleni zitapatikana katika maduka yaliyopo karibu na shule Kwa bei ya shilingi elfu kumi na Tano(15000/=)kila moja ,na Kwa wanafunzi wa kiislamu waje na JUBA ya kushinda ya rangi ya blue bahari ya kitambaa Cha tetroni.

h) Raba nyeupe jozi moja kwa ajili ya michezo pamoja na soksi nyeusi jozi mbili.

i) Viatu vya wazi(sandals)kwa ajili ya kushindia, Mwanafunzi

hataruhusiwa kuvaa ndala wala yeboyebo.Yebo yebo zitatumika bafuni na maliwatoni tu.

j) Mzazi unashauriwa kumpatia mwanao mahitaji ya kutosha kwani hataruhusiwa kutoka nje ya shule kwa muda wote wa masomo.

**KUMBUKA :Mwanafunzi analazimika kuvaa vazi la shule wakati wote awapo shuleni,hivyo asije na nguo za nyumbani.**

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shule ni:-**

k) Madaftari12 au zaidi ya"counter book quire4"
l) Ream(A4) ya Karatasi Mbili(2)kwa mwaka;
m) Vitabu vya masomo ya tahasusi husika.
n) Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;
o) Scientific Calculator kwa wanafunzi wote wa Sayansi
p) Godoro kwa wanafunzi wote liwe na ukubwa kulingana na vipimo vilivyopo shuleni .Size ya godoro ni 6 x2.5x6"na kila mwanafunzi atapaswa kuja na godoro lake.Kwa atakayeshindwa kuja na godoro atalazimika kununua godoro katika maduka yaliyo jirani na shule Kwa gharama ya TSH 50,000/=.

q) Mashuka Jozi 2 yenye rangi ya pinki na blanket 1jeusi, foronya ya rangi ya shule 1,chandarua1chenye rangi nyeupe.
r) Nguo za ndani za kutosha .
s) Taulo, na vitenge au kanga jozi moja atajifunga wakati wa kwenda kuoga.
t) Vyombo vya chakula (sahani,bakuli,kijiko na kikombe);
u) Ndoo2 kubwa moja na ndogo(lita 10 na ishirini)zenye mifuniko;
v) Mopper 1 , jembe 1, fagio ngumu(hard broom) 1, mifagio 2 wa ndani na nje kwa wanafunzi wote.
w) Sabuni lita
x) Bima ya afya.Na endapo mwanafunzi hatakuwa nayo atalazimika kupatiwa bima ya jamii ya CHF Kwa gharama ya Tsh 5000/=.

a)Mwanafunzi asije na mizigo au begi kubwa shuleni, aje naTranka moja tu .

b)Hairuhusiwi mwanafunzi kutembelewa na wageni wakati wote atakaokuwa shuleni ISIPOKUWA kwa wito iwapo italazimika. Siku ya kuwaona wanafunzi ni siku ya mahafali ya kidato cha Sita.

c)Ni muhimu kwa mzazi/mlezi kutoa nafasi kwa walimu kufanya kazi zao bila usumbufu kwa kumshirikisha mwanafunzi mambo yasiyo na tija kwake akiwa shuleni.

**Michango mbalimbali**

| Na | Aina yaMchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | MchangowaUendeshajiwaShule | 65,000.00 |
| 3. | Tahadhari | 5,000.00 |
| 4. | Nembo | 5,000.00 |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000.00 |
| **Jumla** | | **80,000.00** |

Malipo yote yalipwe kupitia Benki ya NMB tawi lolote au Wakala yeyote nchini kwa kupitia akaunti namba **50201200071** yenye jina la **'Mondo Secondary School'.** Stakabadhi zote za malipo (bank pay-in-slip) ziletweShuleni zikiwa na jina la mwanafunzi,kidato na tahasusi yake nyuma.

**ANGALIZO**:Shule haitahusika na malipo yoyote yatakayofanywa bila kupitia benki.

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa SheriaNa.10 ya mwaka1995 Aidha,inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu,SayansinaTeknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.Mambo hayo ni pamoja na;

### Sheria na Kanuni za Shule

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;

b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
c) Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku(Preparation);
d) Kuwahikatika kilashughulizashuleutakazopewa;
e) Kufahamu mipakaya shule nakuzingatia kikamilifu maelekezo yakuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
f) Kutunza usafi wa mwili,mavazi na mazingira ya shule;
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
i) Kutunza mali za shule;
j) Nimarufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye nchakali na dawa bila idhini ya daktari;na
k) Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa.Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule.(Msiba au Ugonjwa**).

**Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

a) Wizi;
b) Kutohudhuria masomo kwazaidi siku90 bila taarifa/utoro;
c) Kugoma nakuhamasisha mgomo;
d) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi najamii kwaujumla;
e) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
f) Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.Haturuhusu kusuka nywele.
g) Kufuga ndevu;
h) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;

i) Uvutaji wa sigara;

j) Uasherati,mahusiano ya jinsia moja,kuoa au kuolewa;
k) Kupata ujauzito au kutoa mimba;

l) Kushiriki matendo ya uhalifu,siasa,na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
m) Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
n) Kumiliki,kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
o) Kudharau Bendera yaTaifa;
q) Kufanya jaribio lolote la kujiua,au kutishia kujiua kama kunywa sumu na,
q )Uharibifu wamali ya umma kwa makusudi.

**3.3 Viambatisho naFomuMuhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wakutoshiriki katika migomo,fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule;na
iv. Picha nne(4)za wazazi na ndugu wakaribu wamwanafunzi wanaonaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**4.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA SHULENI HAPA**

**...............................**

# ALWINO ALOIS LUWUNGO

## MKUU WA SHULE

**NB:Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli(wizikwanjiayamitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atumepesa.TAFADHALIUPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWANAMBA ZIFUATAZO:-**

- **Mkuuwashule:0788605075 (mwl.Alwino Alois Luwungo)**
- **MakamuMkuuwaShule:0786226927 (Mwl.Shamani Sudi)**
- **MwandamiziTaaluma:0785060949(mwl.Kalist Severini)**
- **MwandamiziMalezi:0752582235(mwl.Devotha Philipo)**

Mwalimuwa usajili:0752582235(mwl.Devotha Phili

...      .      **FomuNa.1**

**AHADI YA MZAZI/MLEZI**

Mimi_______________________wa S.L.P_Mji________________Simu ______________na mwenye picha hapo juu. Ambaye kazi yangu ni _______________natamkahapakamamzazi/mleziwa_ _______________.Ninakubalikwahiari yangu mwanangu asome katika Shule ya Sekondari Mondo kuanzia tarehe____________.Nina ahidi kama ifuatavyo:-

1. Kwamba nimekubali chaguo alilopewa mwanangu na sitamruhusu kubadilisha hadi apate kibali chamaandishi kutoka kwa mamlaka husika.
2. Ninaahidi kumpatia mwanangu vifaa vyote kama vilivyoainishwa katika fomu ya kujiunga ikiwemo SAREKAMILI ya shule bila kuharibu chochote.
3. Ninatambua ya kuwa walimu wanahitaji ushirikiano wangu katika kumpatia mwanangu elimu na nitashirikiana nao bega kwa bega kwa masuala yanayomuhusu mwanangu kitaaluma na nidhamu ili aweze kufikia malengo yake na yaTaifa.

1. Naahidi kuwa endapo mwanangu ataenda kinyume na taratibu zilizoainishwa katika fomu hii achukuliwe hatua stahili za kinidhamu kama zilivyoorodheshewa.

Jina:____________________________ saini__________________

Tarehe:______________Uhusianona mwanafunzi:______________

**FomuNa.2**

**AHADI YA MWANAFUNZI**

Mimi mwanafunzi________________________________Wa kidato chaTano chaguo(tahasusi)______mwakawamasomo2024/2025 .Ninakiri kusoma,kuelewa na kuahidi kutii taratibu zote zilizoainishwa katika fomu iliyotumwa kwangu na Mkuu wa shule ya Sekondari Mondo. Nitatoa ushirikianowa kutosha kwa walimu wangu na shule kwa ujumla katika muda wangu wote nitakaokuwa shuleni ili niweze kupata elimu nakuendeleza jamii naTaifa langu.

Jina:____________________________ Saini________________

Tarehe:____________________

**FomuNa.3**

**KIAPOCHAMZAZI/MLEZI**

Mimi:____________________wa S.L.P______________Mji_Simu Na____________. Nakiri kukaa na kuzungumza na mwanangu juu ya taratibu nasheria za shule na ninaahidi kumsaidia na kutoa ushirikiano wa kutosha kwa Mkuuwa Shule na walimu kwa muda wote ambao mwanangu atakapokuwa katika shulehii. Ninatambua madhara ya mwanangu kutembelewa na wageni wasioeleweka wakati akiwa shuleni naomba shule iwatambue watu watatu(3) ambao wanahusaka katika muda wote ambao atakuwa shuleni nao ni:-(ambatanisha passport size zao).

*Picha yandugu waKwanz*

Jina:______________________________ Kazi:______________ Makazi: _________________ Simu:______________________ ____________________________________________________Uhusianonamwanafunzi:________________________________________

*Picha yandugu*

Jina:____________________________________________ Kazi:_________ Makazi:___________________ Simu:_______________ Uhusiano na mwanafunzi:__________________________________________

*Picha*

Jina:________________________________ Makazi:
Simu:------------------------- Uhusiano na mwanafunzi:____________________

**FomuNa4**

**UTHIBITISHO WAAFYA**

Mondo sec School,
P.O.BOX88
Mondo.

Student's photo

**MEDICALEXAMINATIONFORM**

TobecompletedbyMedicalOfficerfromaknownPublicHospitalorHealthCentrein respecttoallentrants

Fullname……………………...…………..Age……...Sex…………year…....

1. Bloodcount(RedandWhite)………………………………………...
2. UrinalysisTest………………………………………………….
3. Syphilistest……………………………………………………
4. T.B……………………………………………………………
5. EyeTest……………………………………………………
6. Ears……………………………………………………………
7. Spleen…………………………………………………………
8. Abdomen…………………………………………………….

ADDITIONALINFORMATION:e.g.Physicalimpairment,familydisease,chronicinf ectionsetc.

……………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………

Icertifythattheabovenamedindividualisfittopursuestudiesasstatedabove

………………………………..

…………………………………….

NameandDesignation SignatureandOfficialstamp

……………………………….. ……………………………

DATE

**NOTE:**

1. *Medicalofficerduringthecourseofthis Examinationpleaseattendtheindividualaccordingtoanydiagnosedcas e.*
2. *ThedullyfilledformmustbehandedtotheHeadoftheSchoolduringregistrationweek,underNocircumstancess hould astudent beregisteredwithout certificationofhis/herphysicalfitness.*